MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA


**Na: 21. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Aprili 11-20, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 21-30, 2019**

**Muhtasari**

- Mazao yanaendelea vizuri katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka kutokana na mvua za Msimu zinazoendelea
- Ukuaji wa mazao kwa maeneo ya Kanda ya Kati umeathiriwa kutokana na upungufu wa mvua kwa muda mrefu wa msimu
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza uzalishaji wenye tija kutokana na hali ya hewa inayotarajiwa.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika na ile iliyopo kusini, (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hii ilisababisha msukumo wa ukanda wa mvua (Inter Tropical Convergence Zone (ITCZ)) kuwepo katika maeneo mengi ya Tanzania. Katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikua juu ya wastani hivyo kuchangia katika kufanyika kwa mgandamizo mdogo wa hali ya hewa nje kidogo ya bahari Tanzania. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilikuwa katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii iliweza kusababisha mvua katika maeneo kadhaa ya nchi.




Kielelezo:1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha April 11- 20, 2019.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa katika kipindi cha dekadi, mvua ziliendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, kusini, pwani ya kusini, ukanda wa Pwani, kanda ya ziwa Victoria na magharibi. Maeneo haya yalipata mvua kati ya mm 26 na 100. Hata hivyo, maeneo ya mkoa wa Ruvuma, Mara, na Morogoro yalipata mvua za zaidi ya mm 150. Maeneo mengine hususan kanda ya kati na nyanda za juu kaskazini mashariki yalipata mvua chini ya mm 10 kama Kielelezo kinavyoonyesha.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019

Mazao yanaendelea vizuri katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hususan mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa, na Ruvuma kutokana na mvua za msimu zinazoendelea. Zao la mahindi lilikuwa kwenye hatua ya kukomaa. Hata hiyvo kutokana na upungufu wa mvua katika maeneo ya kanda kati na kusini mwa mkoa wa Manyara imepelekea mazao hususani mahindi kunyauka. Kwa upande mwingine maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan Pwani ya Kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki, vipindi vya ukavu baada ya msimu wa mvua kuanza vimesababisha kuchelewa kupanda au kutokupanda kabisa mazao ya msimu wa Masika. Mikoa ya Tanga, Pwani na Morogoro, mahindi yalikuwa katika hatua ya jani la tatu wakati mikoa ya Shinyanga na Mwanza wakulima wanaendelea na shughuli za uvunaji wa mazao ya msimu wa Vuli 2018. Hata hivyo mkoa wa Kagera hususan wilaya ya Bukoba iliendelea kupata mvua za wastani ambazo zimesaidia ukuaji wa mazao. Wakulima katika maeneo haya wanaendela na

palizi. Upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo ulikua katika hali nzuri kwa maeneo mengi ya nchi.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mitiririko ya maji kwenye mito kwa maeneo yaliyoendelea kupata mvua viliendelea kuimarika kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kudhoofika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususani maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Joto la bahari la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo inaweza kupelekea ongezeko la mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani katika ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi ya Tanzania.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) kunatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo. Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache. Maeneo ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla na uwezekano wa mvua nyepesi katika maeneo machache zinatarajiwa. Maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache. Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) kunatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30,2019

Unyevunyevu kwenye udongo unatarajiwa kuongezeka hususan katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, pwani ya kusini, kanda wa ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya kaskazini, maeneo ya kusini na magharibi mwa nchi kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hali hii itasaidia ukuaji wa mazao. Hata hivyo, mazao ya muda mfupi ndio yanayoshauriwa kwa msimu huu ambao ni mfupi na wenye vipindi virefu vya ukavu. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza tija kutokana na hali ya hewa inayotarajiwa.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2019

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu licha ya ongezeko lililotabiriwa.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***